

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### 1. Hali ya upatikanaji wa mbolea katika Mkoa wa Ruvuma

Katika msimu wa kilimo 2019/2020 wakulima wameitikia kilimo kwa kuongeza ukubwa wa mashamba na kutumia teknolojia pamoja na mbinu za kilimo bora. Hali hii imechochewa na bei nzuri ya mazao ya msimu 2018/2019. Mbolea nyingine zimeendelea kupatikana isipokuwa UREA imeonekana kuhitajika kwa wingi.

### 2. Upungufu wa mbolea ya UREA

Katika msimu huu wa 2019/2020 kumekuwa na ongezeko la matumizi ya mbolea za kukuzia aina ya UREA. Juhudi kubwa za ufumbuzi zimefanwa na Serikali kwa kuingiza meli za mbolea kwa awamu tofauti. Meli ya kwanza ilishusha tani elfu 10 mwezi Januari 2020 ambazo zilisambazwa kwa wakulima na meli ya pili inaendelea kushusha jumla tani elfu 43 katika bandari ya Dar es salam ambazo ambazo zitafika kwa wakulima mwanzoni mwa mwezi Februari 2020.

Wafanyabiashara wa mbolea wa Mkoa wa Ruvuma wanaaswa kwenda Dar es salaam kuchukua mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa kuzingatia sheria kanuni na miongozo.

### 3. Matumizi ya mbolea mbadala

Mkulima anashauriwa kutumia mbolea mdadala kukuzia mazao yake endapo mbolea ya **UREA** itakuwa haipo sokoni. Mbolea hizo ni SA, CAN, Minjingu Top-Up, YARA Cereal, YARA Amidas na YARA Sulfan.

### 4. Usimamizi wa bei elekezi za mbolea

Mkoa wa Ruvuma na halmashauri zake umepewa jukumu la kusimamia mwenendo wa bei za mbolea kwa mujibu wa sheria ya mbolea ya mwaka 2009 na kanuni zake kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2011 na 2017.

Mbolea zinazohusika katika manunuzi ya mbolea kwa pamoja (BPS) ni UREA na DAP. Bei hupangwa kwa kuzingatia umbali wa maeneo ya pembezoni kama majedwali yanavyoonekana;

**(i). Bei elekezi za mbolea UREA Msimu 2019/2020**

<b>Na</b>	<b>Halmashauri</b>	<b>Bei ya rejareja (TSh) - mkulima</b>	<b>Bei ya jumla (TSh) - mfanyabiashara</b>
1	MADABA (Mtyangimbole)	55,195	52,663
2	MBINGA DC (Muungano)	56,424	53,836
3	MBINGA TC (Kihungu)	55,854	53292
4	NATUMBO DC (Magazini)	56,364	53,778
5	NYASA DC (Mipotopoto)	56,844	54,236
6	SONGEA DC (Lilahi)	55,531	52,983
7	SONGEA MC (Mwengemshindo)	55,195	52,663
8	TUNDURU (Kalulu Via Lindi)	54,775	52,263

**(ii). Bei elekezi za mbolea DAP MSIMU 2019/2020**

<b>Na</b>	<b>Halmashauri</b>	<b>Bei ya rejareja (TSh)</b>	<b>Bei ya jumla (TSh)</b>
1	MADABA (Mtyangimbole)	<b>59,663</b>	56,348
2	MBINGA DC (Muungano)	<b>60,881</b>	57,498
3	MBINGA TC (Kihungu)	<b>60,316</b>	56,965
4	NATUMBO DC (Magazini)	<b>60,821</b>	57,442
5	NYASA DC (Mipotopoto)	<b>61,296</b>	57,891
6	SONGEA DC (Lilahi)	<b>59,996</b>	56,662
7	SONGEA MC (Mwengemshindo)	<b>59,663</b>	56,348
8	TUNDURU (Kalulu Via Lindi)	<b>59,247</b>	55,956

## **5. Kufungua mifuko**

Kumetokea tabia ya watu kufungua na kuuza kwa kupima mbolea kwa watumiaji wadogo ya mazao ya bustani. Hairuhusiwi kufungua mifuko ya mbolea na kuipima kwani inaharibu ubora wa mbolea. Mbolea hupoteza ubora kupitia mvuke na kubaki makapi mabayo hayafai kwa mmea.

Hilo ni kosa na atakayebainika itampasa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria ili apate adhabu ya kufungwa au kulipa faini kwa mujibu wa sheria.

Onesmo Kenani Ngao  
**AFISA KILIMO – RS RUVUMA**  
**29/01/2020**